

## Wapi naweza kupata Fomu na kijitabu cha Advance Care Directive?

Fomu na Kijitabu cha Advance Care Directive vinaweza kupatikana kwenye mtandao kwa bure kwenye:

**[www.advancecaredirectives.sa.gov.au](http://www.advancecaredirectives.sa.gov.au)**

Unaweza pia kujaza toleo la kisasa kwa kujaza Fomu ya kwenye Mtandao ambayo itakuelekeza wazi.

Nakala ya karatasi yenye Fomu na Kijitabu inaweza kuombwa kwenye tovuti ya Advance Care Directive au unaweza kupigia Service SA kwa 13 23 24 wakati wa masaa ya kazi ili wakutumie moja.



## Kwa habari zaidi

Tovuti ya Advance Care Directive ina maelezo ya ziada, karatasi za ukweli, rasilimali na viungo vya kukusaidia kujaza Fomu yako ya Advanced Care Directive.

Tembelea

**[www.advancecaredirectives.sa.gov.au](http://www.advancecaredirectives.sa.gov.au)**

na kufanya matakwa yako ya afya na maamuzi ya kimaisha kuwa wazi.

Kamishna ya Huduma za Sheria inaweza kukupa ushauri na uwakili kwa Fomu yako ya Advance Care Directive.

Simu

**1300 366 424**

Tovuti

**[www.lsc.sa.gov.au](http://www.lsc.sa.gov.au)**



# Fanya matakwa yako ya huduma kuwa wazi leo, ikitokea huwezi kesho.

Advance Care Directive inawapa wale wanao kutunza ufahamu wa wazi wa mahitaji yako na matakwa kama ukipoteza uwezo wa kuwasiliana nao mwenyewe.



 **Advance Care Directive**  
matakwa yako kwa huduma ya baadaye

Kunaweza kuwa na md ambapo huwezi kufanya maamuzi au kuwasiliana vizuri juu ya matakwa yako juu ya jinsi gani ungependa kutunzwa au kuchukuliwa.

Hii inaweza kujumuisha sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- ajali au madhara ya afya kiakili
- shida ya akili au hali kama hiyo
- ugojwa wa kiarusi wa ghafla
- kwa sababu huna ufahamu au katika kupoteza fahamu.

Hii inaweza kutokea katika umri wowote au hatua ya maisha. Kama ikitokea, ungependa maamuzi yafanyike namnagani kwa ajili yako kuhusu huduma zako za afya za kuendelea, mipango ya kuishi na mambo mengine binafsi? watu gani ungependa wafanye maamuzi hayo kwa ajili yako?



## Advance Care Directive

Advance Care Directive mpya ni hatua mhimu ya kuendelea kupangilia afya yako.

Advance Care Directive mpya inarudiria ile iliyokuwepo ya Kupata Nguvu ya Usimamizi, Nguvu ya Mwanasheria na Mwelekeo Tegemezi kwa kuwa na fomu moja ya Advance Care Directive.

## Itaniruhusu mimi kufanya nini?

Advance Care Directive mpya inakuruhusu ku:

- kuandika matakwa yako, mapendekezo na maelekezo ya huduma yako ya afya baadaye, mwisho wa maisha, mipango ya kuishi na mambo ya kibinafsi; na / au
- kuteua mtu mmoja au zaidi wa Mbadala Kufanya Maamuzi ili afanye maamuzi haya kwa niaba yako, kama wewe ukishindwa kuyafanya mwenyewe

## Kwa nini niwe na mtu?

Itakupa amani ya akili kwamba wale wanaokutunza watakuwa wanajua ni nini unataka, wakati wewe hauwezi kufanya maamuzi yako mwenyewe au kuwasiliana matakwa yako na maadili.



## Kijitabu kina nini?

Kijitabu kina Fomu ya Advanced Care Directive na hatua kwa hatua ya mwongozo ambao unakupa kila kitu unahitaji kukamilisha fomu yako ya Advance Care Directive.

Hii inajumuisha: mifano ya kauli, habari kwa Wafanya Maamuzi-Mbadalai, mashahidi na wakalimani, karatasi za ukweli na rasilimali zingine na maelekezo.